**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA**

**SHULE YA SEKONDARI VUDOI**
**S.L.P 157**
**Barua pepe** vudoisekondari school@yahoo.com
**14/06/2023**

Unapojibu tafadhali taja,
**Kumb. Na. VSS/K.2021/VOL.I/V**
**Simu Na. 0687 786992/0736 786992**
**0759379856/0719180369**

**KWA MWANAFUNZI:** ……………………...………………………………………………
**S. L. P.** ………….… **WILAYA …**……………………………**MKOA WA** ………………………

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI VUDOI, KIDATO CHA TANO MKONDO WA HGL, HKL, HGK**

## 0.0. UTANGULIZI

Ninayofuraha kukuarifu kwamba, umechaguliwa kujiunga na kidato cha TANO katika shule hii mwaka 2023. Shule ya sekondari Vudoi ipo umbali wa Km 2 mashariki mwa barabara kuu ya DSM na Arusha karibu na makazi ya polisi Mwanga. Unaweza kushuka stendi kuu ya mabasi Mwanga na ukafika Vudoi bila shida yoyote. Usafiri wa teksi kutoka mjini kuja Vudoi unapatikana katika kituo cha mabasi cha mwanga nauli ni Tsh. 4,000/= tu.

Muhula wa kuanza masomo na tarehe za kuripoti shuleni **ni tarehe 13/08/2023 mpaka tarehe 30/08/2023** kama ulivyotangaziwa na serikali na si vinginevyo na kama hujafika basi utakuwa umepoteza nafasi hiyo.

Tafadhali soma kwa makini sana maelekezo / maagizo yafuatayo na ukamilishe mahitaji yote yaliyomo katika fomu hii ili uweze kupokelewa shuleni na kuanza masomo bila usumbufu wowote.

**VIAMBATANISHO MUHIMU:**

- ✓ Fomu **A** ya kukubali kufuata sheria zote na masharti yote ya shule na mkataba wa kutoshiriki migomo fujo zozote na makosa ya jinai ya aina yoyote awapo shuleni.
- ✓ Fomu **B** ya mzazi / mlezi ya uthibitisho wa kulipa ada, michango na mahitaji mengine ya shule kwa wakati.
- ✓ Fomu **C** ya siri inayohusu maelezo binafsi ya mwanafunzi.
- ✓ Fomu ya kupimwa afya na Daktari wa Hospitali ya Wilaya /kituo cha afya cha serikali.
- ✓ Fomu **E** ya usajili wa mwanafunzi (itajazwa shuleni wakati wa kuripoti

## 1.0. Mahitaji muhimu

### A. Sare za shule

- Suruali za shule mbili rangi ya kijivu.
- Sweta moja rangi ya kijivu (inayofanana na rangi ya suruali)
- Shati mbili nyeupe mikono mirefu
- Soksi jozi mbli (2) nyeusi (nunua mwenyewe)
- Viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba visigino vifupi (ujinunulie)
- Suruali ya kushindia rangi nyeusi mbili ashone mwenyewe
- Tshirt ya kushindia itapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh. 12,000/=
- Sare za michezo jezi ya timu ya taifa rangi ya bluu nunua mwenyewe
- Track suit dark bluu kwa ajili ya kuvaa nyakati za jioni
- Raba za michezo jozi moja
- Bukta ya michezo rangi ya bluu
- Mkanda mweusi wa ngozi kwa ajili ya kufunga suruali – upana si zaidi ya inchi moja na nusu na usiwe na chuma kipana / kikubwa cha kufungia na kisiwe na picha au mchoro wowote.

***MASHONO:* Suruali zishonwe vizuri, ziwe na mifuko miwili mbele isiyo ya kuchimba na mmoja wa nyuma usio wa kubandika, marinda 2 mbele kila upande, ziwe na mkunjo wa chini (turn-up), luksi za mkanda zisiwe pana, suruali zisibane kwa chini wala zisiwe peckos. Ni marufuku kabisa kuvaa suruali inayoshika maungo ya mwili (inayobana). Ukileta itachanwa. Hii ni kwa suruali zote hata za binafsi za kushindia. Mashono ya suruali yazingatie kuwa inavaliwa kiunoni na sio mlegezo kidogo.**

### B. VIFAA VYA BWENI

i) Godoro la sponchi ft 2.5 upana na urefu futi 6
ii) Shuka mbili rangi ya pink na mto na foronya, blanketi moja
iii) Sanduku la chuma kwa usalama wa vifaa vyake na kufuli lake imara (SOLEX).
iv) Taulo, sabuni ya unga na za kuogea, mswaki na dawa rangi ya viatu za kutosha
v) Sahani, kijiko na kikombe
vi) Chandarua rangi ya bluu
vii) Kandambili
viii) Tochi na betrii zake kwa ajili ya tahadhari umeme ukatikapo isiwe ya kutumia umeme.
ix) Uje na bima ya afya au fedha kiasi cha Tsh. 6000/= za bima ya ICHF

### C. VIFAA VYA TAALUMA

i) Daftari 07 kubwa (counter book three quire) kalamu ya bluu au nyeusi, penseli na rula
ii) Mkebe (mathematical instruments set) kwa wanaosoma geography
iii) Ream mbili nyeupe A-4 na ruled mbili (kwa ajili ya mazoezi atakabidhi shuleni mara tu atakaporipoti .
iv) (English to English) dictionary (kamusi ya kingereza) vitabu vingine vya kingereza
v) Kamusi ya kiswahili na vitabu vya Kiswahili (kwa wanaosoma kiswhili)
vi) Vitabu vya geography (kwa wale wanaosoma geography)
vii) Vitabu vya history (kwa wale wanaosoma history)
viii) Njoo na nakala ya Leaving Certificate na Result Slip
ix) Stepler machine moja kwa ajili ya kubania kazi zake

## D.MICHANGO YA SHULE

| NO | MCHANGO KWA MWAKA | KIASI CHA TSH |
|---|---|---|
| 1. | Uendeshaji wa shule | 65,000/= kwa mwaka |
| 2. | Kitambulisho /picha | 5,000/= kwa muda wote wa masomo |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= kwa mwaka |
| 4. | Nembo | 5,000/= kwa muda wote wa masomo |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Malipo hayo yafanyike kupitia benk Akaunti **No. 40201100005 NMB A**/C jina la akaunti ni **VUDOI SEKONDARI** kisha ulete risiti kutoka benki uliolipia malipo hayo ya shule na ukumbuke kuiandika jina la mwanafunzi husika. **Michango yote hiyo hapo juu inalipwa mara moja tu unaporipoti .**

## E.MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

i) **RUHUSA: -** Ruhusa ya kutokuwepo shuleni kwa siku moja au zaidi itatolewa na Mkuu wa shule, Makamu wake au Mwalimu aliyekasimiwa madaraka.

ii) **MWOMBEZI WA RUHUSA:-** Anayekubalika kukuombea ruhusa ni mzazi/mlezi aliyeandikishwa shuleni na sio mtu mwingine yeyote.

iii) **MIPAKA YA SHULE:-** Ni marufuku kutoka nje ya mipaka ya shule wakati wote wa masomo/shughuli zingine bila idhini ya mwalimu husika.

iv) **LUGHA RASMI:-** Unatakiwa kutumia lugha ya kiingereza tu mahali popote shuleni. Mawasiliano kati yako na walimu na wanafunzi wenzako yafanyike kwa lugha ya kiingereza.

**UMEME:-** Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kugusa wala kukaribia miundombinu ya umeme mfano: swichi, soketi, taa, swichi kuu wala mita bila sababu za msingi. Tendo la kuwasha taa. Lifanywe mara moja tu sio kubonyeza bonyeza. Nikosa kujiunganishia nyaya za umeme kwa matumizi yoyote yasiyo rasmi, ukikamatwa utafukuzwa shule mara moja. Ukihurumiwa, utaleta roll ya waya 2.5 mm mita 100 pamoja na gharama ya fundi.

**USAFI BINAFSI:-**

- ✓ Ni lazima mwanafunzi awe msafi na nadhifu wakati wote.
- ✓ Mwanafunzi haruhusiwi kufuga ndevu, nywele ndefu wala kusuka kwa namna yoyote ile.
- ✓ Ni marufuku pia kunyoa nywele zote na kubaki na upara. Nywele ziruhusu kijiti cha kiberiti kukaa bila kudondoka.
- ✓ Kucha za miguu na mikono sharti ziwe fupi na zisipakwe rangi yoyote.
- ✓ Sare ya shule ni lazima iwe safi na iliyonyooshwa vizuri. Viatu pia vipakwe rangi yake.
- ✓ **Suruali zitavaliwa kiunoni na sio katikati ya makalio ("kata k").** Mikanda mipana yenye chuma kubwa sehemu ya kufungia na yenye mapichapicha haikubaliki shuleni.
- ✓ Ni lazima uoge mwili mzima ili kuzuia harufu mbaya.
- ✓ Ni marufuku kujipaka / kujipulizia manukato makali wakati wa darasani.

.

**VIFAA KWA AJILI YA USAFI WA MAZINGIRA UTUNZAJI WA MAZINGIRA**

Vikabidhiwe shuleni siku ya kuripoti mwanafunzi

i) Ndoo kubwa Lt 20 moja na ndogo lita 10 (kubwa atakabidhi shuleni) na ndogo ni kwa matumizi ya matumizi yake binafsi.
ii) Fagio za chelewa ya wima 02
iii) Soft broom 01
iv) Squiza 01
v) Mopa nan doo yake
vi) Slesha 01
vii) Dawa ya chooni lita 05 (Aina ya Dexi All-purpose cleaner)
viii) Hard broom 01

**USAFI WA MAZINGIRA NA USAFI**

- Ni wajibu wako kuliweka eneo la shule, majengo na madarasa katika hali ya usafi. Hairuhusiwikuchora chora wala kuandika katika kuta za majengo ya shule.
- Uchafu na takataka zitupwe mahali panapostahili.
- Ni jukumu la kila mwanafunzi kupendezesha maeneo ya shule yetu ili yavutie.

**SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:**

**Mkuu wa shule 0687 786992**

- **Makamu Mkuu wa Shule 0759379856**
- **Mwandamizi Taaluma 0769968933**
- **Mwandamizi Malezi 0785835674**

**D. TANBIHI: Pamoja na maagizo haya, tafadhali tekeleza yafuatayo:-**

Tuandikie tujulishe rasmi kukubali kufuata sheria za shule hii kwa kujaza fomu A kwa ukamilifu. iliyoambatanishwa na uirejeshe siku ya kuripoti shuleni.

- Jaza fomu **B** inayohusu uthibitisho wa kulipa ada na uirejeshe siku ya kuripoti.
- Jaza fomu **C** inayohusu maelezo binafsi ya mwanafunzi (Fomu ya siri) na uiwasilishe kwa mkuu wa shule siku ya kuripoti.
- Jaza fomu **D** (ripoti ya Daktari) – ijazwe na Hospitali yenye hadhi ya Kituo cha afya , wilaya au mkoa na sio zahanati na pia iletwe siku ya kuripoti.
- Fomu **E** inahusu usajili **-** Itajazwa na kila mmoja baada ya kuonyesha mahitaji na michango yote wakati wa kuripoti shuleni.
- Hakikisha unaandika jina lako kwa kudarizi katika sare zote, shuka, track suit na blanketi.

**MWISHO:** Kwa niaba ya bodi ya shule walimu na wafanyakazi wote, nakupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na shule yetu. Na Imani yetu kuwa utaitumia vizuri nafasi hii uliyotunukiwa na Taifa.

**KARIBU SANA VUDOI SEKONDARI**

Ahsante

HEAD OF SCHOOL
VUDOI SECONDARY SCHOOL
P. O. Box 157 MWANGA

**O.M.MBELENJE**
**MKUU WA SHULE**

**HATI YA MAKUBALIANO/MKATABA**
**KUKUBALI KUFUATA SHERIA NA MASHARTI YA SHULE**

Picha ya mwanafunzi

**A. HABARI ZA WAZAZI/WALEZI NA WANAFUNZI**

**SEHEMU A: (TAARIFA ZA MWANAFUNZI)**

1. Jina kamili (kama kwenye mtihani) …………………………………….
2. Tarehe ya kuzaliwa…………………………………Dini…………………
3. Mahali na wilaya alipozaliwa……………………………………………
4. Shule uliomaliza darasa la saba……………………………………….
   Mwaka uliomaliza………………………….
5. Kidato chako unachokuja kuingia hapa shule ya sekondari Vudoi ………………….
6. Matatizo ya afya uliyonayo mwanafunzi…………………………………………..

Picha ya mzazi/mlezi

**B. TAARIFA ZA MAZAZI/MLEZI**

i) Jina kamili la mzazi/mlezi …………………………………………….
ii) Mahali anapoishi……………………………………………………….
iii) Wadhifa/kazi yake…………………………………………………
iv) Mahali anapofanya kazi……………………………………………
v) Namba za simu za mzazi/mlezi……………………………………..
vi) Namba za simu za mtu mwingine wa karibu…………………………..

**C. AHADI YA UTII/TABIA NJEMA**

Mimi……………………………………………..(Jina kamili la mwanafunzi) wa kidato cha….naahidi mbele ya mzazi/mlezi wangu na mbele ya mkuu wa shule.

a) Kwamba nitafuata sheria na kanuni za shule pamoja na maelekezo yote halali yanayotolewa mara kwa mara na uongozi wa shule
b) Kwamba nitatii
c) Kwamba sitatoka nje ya mipaka ya shule labda tu kwa ruhusa maalumu kwa mwalimu wa zamu, mwalimu mlezi, makamu mkuu wa shule au mkuu wa shule mwenyewe
d) Kwamba sitamiliki simu ya mkononi wala laini ya simu wala kifaa chochote kinachotumia umeme.
e) Kwamba kama nitashindwa kufuata au kuzingatia maadili mema nipewayo na walezi wangu shuleni hatua kali zichuliwe dhidi yangu ambayo ni pamoja na kuachishwa masomo.


**D. AHADI YA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO/FUJO/KOSA LA JINAI**

Mimi…………………………………(jina kamili la mwanafunzi) wa kidato cha …..mwaka………natambua vema wajibu wangu kwa Taifa kama mwanafunzi kwa hiyo naahidi kutojihusisha na mgomo, fujo au ushawishi wa aina yoyote wa kusababisha mgomo au makusanyiko katika shule. Aidha naahidi kuwa sitashiriki katika makosa yote ya jinai nanikibainika kuchochea ama kushiriki mgomo au jina yoyote basi nifukuzwe shule mara moja.

**AHADI HII NIMETOA LEO TAREHE………………Mwaka………**

| | |
|---|---|
| **JINA LA MZAZI/MLEZI** | **SAHIHI YA MZAZI / MLEZI** |
| **…………………………………….** | **……………………………………** |
| **JINA LA MWANAFUNZI** | **SAHIHI YA MWANAFUNZI** |
| **…………………………………….** | **……………………………………** |

**JINA LA M/KITI WA KIJIJI/MTAA AU MTENDAJI WA KATA**
**……………………………………………………………………**
**TAREHE………………………………………**
**SAHIHI………………………………………**






**O.M.MBELENJE**
**MKUU WA SHULE**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI VUDOI**
**S.L.P 157**
**MWANGA**
**SIMU.0687 786992**

**FOMU B**

**FOMU YA UTHIBITISHO WA KUMPATIA MWANAO MAHITAJI YA SHULE KWA WAKATI**

Mimi……………………………………………………………..mzazi/mlezi wa mwanafunzi………………………………………….(Jina la mwanafunzi) nathibitisha kuwa mwanafunzi huyu aliyechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Vudoi ni mzaliwa wa kijiji cha………..………………....kata ya …………………..………………wilaya ya……………………mkoa wa ……………………..Nitampatia mwanangu mahitaji yote muhimu ya shule mwanzo wa muhula bila kusumbua uongozi wa shule.

| | |
|---|---|
| **…………………………………** | **………………………………** |
| **JINA LA MZAZI/MLEZI** | **SAHIHI YA MZAZI/MLEZI** |
| **TAREHE…………………..** | |
| **…………………………………** | **………………………………** |
| **MTENDAJI/ MWENYEKITI WA KIJIJI** | **MHURI WA KA KIJIJI** |
| **……………………………** | **…………………………………** |
| **MTENDAJI KATA** | **MHURI WA KATA** |
| **TAREHE ……………………** | |

**TANBIHI**

Endapo una mfadhili wa kumlipia mwanao, uthibitishe hapa chini kwa maandishi sahihi na mhuri jinsi atakavyolipa na malipo hayo yafanyike kabla ya mwezi September 2023 ili kurahisisha utendaji

**MFADHILI**

…………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………….

**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

**JAZA FOMU HII KWA UKWELI. HII NI SIRI KATI YAKO NA MKUU WA SHULE TU**

1. **ANDIKA MAJINA KAMILI**
   i) Majina yako halisi……………………………………………………………
   ii) Majina yako ya nyumbani………………………………………………………

| | JINA | BABA | UKOO | UMRI | Tarehe ya kuzaliwa |
|---|---|---|---|---|---|
| LAKO | | | | | |
| BABA | | | | | |
| MAMA | | | | | |

2. **NYUMBANI**
   Kiji/Mtaa……………………………….Kata………………………………………..
   Tarafa………………………………….Mkoa……………………………………..

3. **ANUANI YA NYUMBA**
   ……………………………………………………………………………………….
4. Kukiwa na tatizo taarifa ipelekwe kwa nani……………………………………………………. Uhusiano na wewe…………………………………………………………………………..
   Anafanya kazi gani na wapi?..............……………………………………………..

5. **Wazazi na ndugu.**
   Baba yuko hai?…………………………………………Mama yuko hai?............................
   Baba anao watoto wangapi? …………………………wavulana……….wasichana…………
   Baba ana wake wangapi?.................................................wewe ni mtoto wake wa ngapi……….
   Mko wa ngapi kwa mama yako? …………wewe ni mtoto wangapi kwa mama…………..

6. Dini yako ………………………….…Dhehebu……………………………
   **UNAOWATEGEMEA**
7. (a) Unaishi na nani na wapi?.......................................................................................
   (b) Nani anayekupa mahitaji ya shule? ………………………………………………


   **TOA SABABU KAMA SIO MZAZI …………………………………………………**

**THE PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**VUDOI SECONDARY SCHOOL**
**P.O.BOX 157 MWANGA**
**MOB. 0687 786992/0759379856**

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

To.The Medical Officer
……………………………………..
……………………………………..
…………………………………….

Please examine…………………………………………….(student) as to his fitness to pursue secondary Education without any problems.







**O.M. MBELENJE**
**MKUU WA SHULE**

History: Mental lllness? *Yes/No …………………………………………………Asthma and other allergies? Yes/No. Stool…………………………………………………………………………….……
Urine: Sugar……………………………………Protein……..……………..Cells……………………..
Blood: ESR……………………………FBT-WBC Total………………………Differential………..
……………………………………..Hb…………………………gm/dl BS…………………………….
Vision acuity: Right eye……………………………Left eye………………………………………
Chest: Clinical……………………………………………………
Chest X – ray……………………………………………………

Any physical/mental disability *Yes/No if yes please describe in simple terms
…………………………………………………………………………………………………
I have examined the above named student and found that he/she is *FIT/UNFIT to pursue secondary school education.

**Name of the medical incharge………………………………………Signature………………**

**Date……………………………………………**